

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TATU

20 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 20 APRILI, 2021

I. DUA:

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. MASWALI:

WAZIRI MKUU:

104. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Vijana wa Tanzania watapewa stadi mbalimbali za kuwaongezea ujuzi na maarifa kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa Wananchi Kiuchumi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

105. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Serikali ilitoa Sh.500,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo, lakini kiasi cha Sh.204,000,000/= kilirejeshwa baada ya kufunga Mwaka Julai, 2020:-

- (a) Je, ni lini fedha hizo zitarejeshwa ili ujenzi uendelee;
- (b) Gharama ya ujenzi ni Sh.1,500,000,000/=; Je, ni lini kiasi cha Sh.1,000,000,000/= kitatolewa ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

106. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Jimbo la Mbulu Vijijini ili Vijana wapate ujuzi.

WIZARA YA MAJI:

**107. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA
(MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ya Mto Ruvuma kwa Wananchi wa Mtwara ili kuondoa shida ya maji iliyodumu kwa muda mrefu.

**108. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE
(NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kijiji cha Matandarani Kata ya Sitalike.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**109. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA
(MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ili ifahamike kwa Watalii wa ndani na nje.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

110. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Mbali na kutafuta masoko ya ndani na nje kwa mazao ya Wakulima: -

Je, Serikali ina mkakati gani kupitia SIDO kutengeneza mashine zitakazosaidia kuchakata mazao ya Wakulima, kama vile mashine ya kutengeneza *chips* za Ndizi, Muhogo, *Sauce* za Nyama, Karoti, Pilipili hoho na Mbogamboga kwa gharama nafuu.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

111. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi hadi Nachingwea kwa kiwango cha lami.

112. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Barabara ya kutoka Kibena (Stop

Lupembe) mpaka Madeke C Mfiji, Km 125, imeshafanyiwa usanifu na upembuzi yakinifu tangu Mwaka 2015:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza kwa kiwango cha lami.

113. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Makamu wa Rais kwa Wananchi wa Mbinga ya kujenga barabara ya Mbinga – Litembo – Kigonsera hadi Matiri kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
20 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**